



TAARIFA KWA UMMA

ONYO KWA WANAODHIHAKI FEDHA YA TANZANIA

Benki Kuu ya Tanzania imewataka wananchi kuheshimu Fedha ya Tanzania kwa kuwa ni moja ya alama ya taifa na kuonya kwamba kudhihaki na kukejeli noti na sarafu za Tanzania ni kosa la jinai.

Onyo hilo limetolewa leo kufuatia matukio ya hivi karibuni ya baadhi ya wananchi kutoziheshimu na kuzifanyia dhihaka na kebehi noti za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuzirusha hovyoy na kucheza huku wakizikanyaga kana kwamba ni karatasi za kawaida zisizoheshimika.

Jambo hili ni dharau kwa serikali inayotumia gharama kubwa katika utengenezaji wa noti hizo. Benki kuu ya Tanzania inawakumbusha Wananchi wote kuwa kuharibu noti au sarafu, au kuonesha dharau au dhihaka kwa noti au sarafu za Jamhuri ya Muungano ni kosa la jinai kwa mujibu wa kifungu namba 332A cha Kanuni ya Adhabu (*Penal Code*) Sura ya 16 kama ilivyorejewa mwaka 2002.

Benki Kuu inapenda kuchukua fursa hii kuwatahadharisha wananchi kutojihusisha na vitendo vya aina hii. Endapo ikibainika hatua za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote atakayehusika.

Benki Kuu inatoa rai kwa wananchi kuzitunza fedha zetu kwa kuwa ni mojawapo ya tunu na alama muhimu ya uchumi wa nchi yetu. Vilevile, utunzaji mzuri wa fedha

zetu utapunguza uwezekano wa fedha hizo kuchakaa mapema na kupunguza gharama za uchapishaji.

Kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2006, kifungu cha 26, Benki Kuu ya Tanzania ndiyo taasisi pekee yenye mamlaka ya kutoa noti na sarafu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Noti na sarafu hizo zina alama muhimu inayolitambulisha taifa la Tanzania ambayo ni nembo ya Bwana na Bibi. Alama hii inapaswa kuheshimwa kama zilivyo alama nyingine kwamfano Bendera ya Taifa. Noti na sarafu zote zimetengenezwa kutoa thamani ya kisheria (*legal tender*) kama ilivyoandikwa juu ya noti au sarafu husika na pia Benki Kuu pekee ndiyo yenye mamlaka ya kuharibu noti na sarafu (kifungu cha 28 kikisomwa pamoja na kifungu cha 30 cha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2006).

Imetolewa na:

Idara ya Uhusiano wa Umma na Itifaki botcommunications@bot.go.tz

18 Septemba 2018